



NI NANI ANAYESTAHIKI?

Wakazi wa kipato cha chini ambao ni:

- Kina mama wajawazito au watoto wachanga;
- Watoto wa umri wa 1-18;
- Wazazi na jamaa walezi wa watoto wanaotegemea watu wengine; au
- Watu wazima wa umri wa miaka 19-64, ambao si wajawazito na hawajastajiki kupokea Medicare.

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, { 2 rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

Bima ya Medicaid kwa Kifupi

NINI KINACHOJUMUISHWA?

- Huduma za wagonjwa wanaolazwa na wa kwenda nyumbani
- Huduma za kliniki
- Uchunguzi wa mapema, utambuzi na matibabu ya watoto wa umri usiozidi miaka 21 chini ya Mpango wa Watoto/Vijana
- Dawa, bidhaa na vifaa vya kimatibabu, na pia vifaa kama vile viti vya magurudumu, nk.
- Huduma za maktaba na picha za eksirei
- Huduma ya kinga ya meno na afya, na kutiniwa na madaktari na wataalam wa meno
- Utunzaji katika kituo cha uuguzi
- Utunzaji kupitia wakala wa afya ya nyumbani na utunzaji wa kibinafsi
- Matibabu katika hospitali za akili (kwa watu wa umri usiozidi miaka 21 au wa umri wa 65 na zaidi), vituo vya afya ya akili, na vifaa vya watu waliodumaa kiakili au wenye ulemavu wa kukua
- Huduma za kupanga uzazi
- Kusafirishwa kwenda kuhudhuria miadi ya matibabu, ikijumuisha usafiri wa umma na kurejeshwa pesa za matumizi ya gari la kibinafsi
- Usafiri kwa ambulensi ya dharura kwenda hospitali
- Bidhaa za kukomesha uvutaji sigara kama vile chingamu na vipachiko

Huenda baadhi ya huduma zisijumuishwe kwa sababu ya umri, hali ya kifedha, hali ya kifamilia au mipango ya kuishi. Baadhi ya huduma zinaweza kuwa na malipo madogo saidizi. Hutakuwa na malipo saidizi ikiwa uko katika mpango uliodhibitiwa, isipokuwa malipo madogo zaidi ya huduma za dawa.

WASILIANA NASI:

nystateofhealth.ny.gov | 1-855-355-5777 au TTY 1-800-662-1220

Nitajuaje kuwa mapato yangu yanaziwasha kustahiki kupokea bima ya Medicaid?

Chati iliyo hapa chini inaonyesha kiwango cha mapato unayoweza kupokea kila mwaka na bado ustahiki kupokea bima ya Medicaid.*
Viwango vya mapato vinategemea idadi ya jamaa unaoishi nao.

Viwango vya Mapato ya Kila Mwaka ya 2020				
Ukubwa wa Familia	Mzazi/Mlezi au Wanandoa Wasio na Watoto au Watu wazima wa umri wa miaka 19 na 20 wasioishi na wazazi wao	Watoto Wenye Umri wa miaka 1 - 18	Watu wazima wenye umri wa miaka 19 na 20 wanaoishi na wazazi	Wanawake Wajawazito, Watoto wa Umri wa Chini ya Mwaka 1, au Watoto Wanaostahiki Kupokea Huduma za Upangaji Uzazi
	138% ya FPL	154% ya FPL	155% ya FPL	223% ya FPL
1	\$17,609	\$19,651	\$19,778	\$28,455
2	\$23,792	\$26,550	\$26,722	\$38,446
3	\$29,974	\$33,449	\$33,666	\$48,436
4	\$36,156	\$40,348	\$40,610	\$58,426
5	\$42,339	\$47,248	\$47,554	\$68,417
6	\$48,521	\$54,147	\$54,498	\$78,407
7	\$54,704	\$61,046	\$61,442	\$88,398
8	\$60,886	\$67,945	\$68,386	\$98,388
9	\$67,068	\$74,844	\$75,330	\$108,378
10	\$73,251	\$81,744	\$82,274	\$118,369
Mtu wa Ziada	\$6,183	\$6,900	\$6,944	\$9,991

*Kulingana na Viwango vya Mali vya Shirikisho (FPL) 2020 Viwango vya mapato vinaweza kurekebishwa kila mwaka kulingana na mabadiliko ya FPL.

Gharama ya Medicaid ni ya kiasi gani?

Malipo ya Kila Mwezi: Hakuna malipo ya kila mwezi ya Medicaid.

Kugawana Gharama: Baadhi ya huduma chini ya Medicaid zinahitaji kiwango kidogo cha malipo saidizi, lakini kuna wakati ambapo malipo saidizi hayajitajiki.

Kiasi cha juu zaidi utakachotumia kwa malipo saidizi chini ya Medicaid kwa mwaka mmoja ni takriban \$200.

Ili usome Maswali Yanayoulizwa Sana na Majibu Yake kuhusu Medicaid, tembelea: http://www.health.ny.gov/health_care/medicaid/